# BRELA Jarida

BRELA WAKALA YA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI
ISSN: 00000401 | Toleo la 01 | Aprili-Septemba, 2021

# BRELA yatia fora Maonesho ya Sabasaba Dar

HABARI UK 3




# Bodi ya Ushauri yatakiwa kuondoa vikwazo vya urasimishaji biashara

HABARI UK 2

**ALAMA**
16 SABABU 5 MUHIMU ZA KUSAJILI ALAMA YA BIASHARA

**FAIDA**
18 BRELA NA MCHANGO WAKE KATIKA KUKUZA UCHUMI WA TANZANIA

**USAJILI**
21 ZIFAHAMU FAIDA KUMI ZA KUSAJILI JINA LA BIASHARA

# Yaliyomo

2 Bodi ya Ushauri yatakiwa kuondoa vikwazo vya urasimishaji biashara

3 BRELA yatia fora maonesho ya Sabasaba Dar

4 Watakiwa kujitokeza kwa wingi kwenye maonesho Tanga

5 Mwambe akunwa na utendaji wa BRELA

7 Tanzania kunufaika na Haki Miliki

8 BRELA yatakiwa kuwatafuta wavumbuzi, wabunifu Tanzania

9 Aipongeza BRELA kutoa elimu kwa umma

10 BRELA yawafariji wagonjwa Dar

11 Dodoma watakiwa kuchangamkia elimu ya BRELA

12 Wafanyabiashara wa mifugo Pugu wanolewa

13 BRELA yawapa somo Wabunifu kusajili vumbuzi

14 Mchango wa jina la biashara katika soko la ushindani

16 Sababu 5 muhimu za kusajili Alama ya biashara

18 BRELA na mchango wake katika kukuza uchumi wa Tanzania

21 Zifahamu faida 10 za kusajili Jina la Biashara

## BODI YA UHARIRI

Andrew Mkapa

Tawi Kilumile

Abdul - rahman Songoro

Tulizo Mpina

Neema Kitala

Nehemia Mihayo

Roida Andusamile

Alpha Nuhu (Mhariri Mstaafu- TSN)

BRELA
WAKALA YA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI

# Bodi ya Ushauri yatakiwa kuondoa vikwazo vya urasimishaji biashara




*Waziri wa Viwanda na Biashara Prof. Kitila Mkumbo (aliyeketi katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) mara baada ya uzinduzi wa Bodi hiyo tarehe 30 Agosti, 2021. Kulia kwake ni Mwenyekiti wa Bodi Prof. Neema Mori na kushoto ni Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA Bw. Godfrey Nyaisa. Wajumbe wengine waliosimama kutoka kushoto ni Dkt. Fred Msemwa, Bw. Elias Kalist, Bi. Judith Kadege na Bw. Allen Kasamala*

Na. Christina njovu

Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imetakiwa kuhakikisha kwamba biashara zote zisizo rasmi zinarasimishwa.

Wito huo ulitolewa na Waziri wa Viwanda na Biashara Prof Kitila Mkumbo wakati akizindua Bodi hiyo ya wajumbe watano.

Alisema majukumu ya msingi ya Bodi hiyo ni kumshauri yeye, kusimamia menejimenti ya BRELA na pia kuhakikisha kwamba inaboresha mazingira ya usajili wa biashara nchini bila kuwepo vikwazo.

"Majukumu ya msingi ya Bodi hii ni kunishauri kwenye mambo ya menejimenti ya Taasisi yetu kwa sababu sasa BRELA ni chombo muhimu sana katika mpango mkubwa wa Rais Samia Suluhu Hassan wa kuboresha mazingira ya biashara hapa Tanzania," alisema.

> *"Tunakadiria kwamba tuna takribani biashara ndogondogo na za kati Milioni Tatu, Laki Saba **(3,700,000)**, kati ya hao ni wafanyabiashara Laki moja na Arobaini na nane elfu **(148,000)** pekee ambao ni sawa na asilimia 4% pekee ndizo zilizosajiliwa, hivyo urasimishaji wa biashara unaanza na biashara kusajiliwa na watu kuunda kampuni katika kuongeza ajira,"alifafanua.*

Waziri huyo alisema angependa kuona Bodi hiyo inasimamia urasimishaji wa biashara hapa nchini kwa kuwa Tanzania ina biashara nyingi zisizo rasmi.

Alisema ili nchi izalishe ajira ni lazima biashara zinarasimishwa na watu walipe kodi na biashara zao zikidhi vigezo vya kupata mikopo kutoka kwenye benki na Taasisi nyingine za fedha.

Prof. Mkumbo alisema kwamba kwa sasa shughuli za biashara zimeingia katika mtandao kutokana na mazingira ya ugonjwa wa UVIKO-19, hata hivyo tayari BRELA inajiendesha kimtandao zaidi.

Aliiagiza Bodi kushughulikia changamoto ya takwimu za BRELA katika kipindi cha miezi mitatu sambamba na kutengeneza mfumo ambao utawezesha kupata takwimu za makampuni ya biashara hapa nchini.

Bodi ya Ushauri pia iliagizwa kukutana haraka na kufanya uchambuzi kuhusu sheria kadhaa, ikiwemo sheria mama ya kampuni ambayo wadau wamekuwa wakiilalamikia kwa madai kwamba baadhi ya vipengele vyake vimepitwa na wakati.

Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Prof. Neema Mori, aliahidi kuyatekeleza maagizo yote na kutoa ushirikiano kwa Menejimenti ya BRELA.

"Kwa maeneo yote ambayo Mheshimiwa Waziri umeyatamka hapa tumeyapokea kwa mikono miwili na tunaahidi tutatoa ushirikiano mkubwa kwa wafanyakazi wote na tutakuwa katika nafasi ya kukushauri wewe lakini pia menejimenti katika maeneo haya ambayo yametajwa, alisema.

Prof. Mori ni mtaalam wa masuala ya biashara kutoka Shule Kuu ya Biashara ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Wajumbe wengine wa Bodi ni Judith Kadege kutoka Sekta binafsi, Allen Kasambala, kutoka GPSA, Elias Kalist, kutoka Hazina, na Dkt Fred Msemwa, kutoka Watumishi Housing.

Sheria ya Wakala za Serikali ya mwaka 1997 pamoja na marekebisho yake yaliyofanyika mwaka 2009, inampa Waziri wa Viwanda na Biashara mamlaka ya kuteua bodi ya kumshauri kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu taasisi husika.

# BRELA yatia fora maonesho ya Sabasaba Dar




*Baadhi ya watumishi wa BRELA, walioshiriki maonesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara(Sabasaba) wakifurahia ushindi baada ya kushika nafasi ya tatu katika kipengele cha Uwezeshaji Biashara na Uwekezaji*

**Na: Nehemia Mihayo**

Nyota ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) iling'ara katika Maonesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara – Sabasaba - yaliyomalizika Julai 13 mwaka huu katika Uwanja wa Mwalimu Julius Nyerere jijini Dar es Salaam.

Katika maonesho hayo BRELA iliibuka mshindi wa tatu katika kundi la washiriki wa maonesho hayo wanaojihusisha na Uwezeshaji Biashara na Uwekezaji.

Akizungumza baada ya kutangazwa kuwa washindi wa tatu, Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa, alisema kwamba ushindi huo ni chachu kwa ajili ya kuboresha huduma na kuwafikia Watanzania wengi zaidi. "Kwa sasa tunajiandaa na mpango wa kuwafikia wadau wetu waliopo katika mikoa 16. Huu ukiwa ni mwendelezo wa zoezi la kuwafikia wateja wetu popote walipo. Awali tulifika katika mikoa ya Njombe, Singida, Ruvuma, Dodoma, Iringa na Morogoro. Hii yote ni kuwafikia wadau wetu katika maeneo yao kuwahamasisha kuhusu urasimishaji wa biashara, kutoa elimu na kufanya usajili wa papo kwa papo," alisema Bw. Nyaisa.

Tangu kuanza kwa maonesho ya Sabasaba Juni 28 mwaka huu, BRELA ilikuwa ikikutana na wadau wake na kutatua changamoto zao papo kwa papo na kutoa elimu kuhusu huduma zake ili kuwahamasisha wadau wake kurasimisha biashara zao.

# Watakiwa kujitokeza kwa wingi kwenye Maonesho Tanga




*Naibu Waziri wa Wizara ya Viwana na Biashara Mhe. Exaud Kigahe (mwenye tai nyeusi) akipata maelezo kuhusu usajili unaotolewa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), kutoka kwa Afisa Msajili Msaidizi Bi. Maryglory Mmari, alipotembelea banda la Taasisi hiyo, kabla ya ufunguzi rasmi wa Maonesho ya Biashara Tanga, yaliyoanza Mei 28, 2021, katika viwanja vya Mwahako jijini Tanga. Maonesho hayo yaliyofunguliwa na Mhe. Kigahe, yalihitimishwa Juni 6, 2021.*

**Na: Roida Andusamile**

Wafanyabiashara na wajasiriamali wametakiwa kujitokeza kwa wingi katika banda la Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Tanga ili kupata elimu ya kurasimisha biashara zao.

Wito huo ulitolewa mjini Tanga na Afisa Leseni wa BRELA, Bw. Robert Mashika, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusiana na ushiriki wao kwenye maonesho hayo.

Kwa mujibu wa Bw. Mashika, BRELA ilishiriki kwenye maonesho hayo ili kuwasaidia wafanyabiashara na wajasiriamali na watu waliokwishaanza kufanya biashara kurasimisha biashara zao. Kuanzia Mei 28 hadi hadi Juni 6, mwaka huu, BRELA ilitoa huduma mbalimbali ikiwa ni pamoja na kusajili Majina ya Biashara, Kampuni na Alama za Biashara na Huduma, utoaji wa Hataza, leseni za biashara kundi A na leseni za Viwanda.

Huduma nyingine zilikuwa ni uhuishaji wa taarifa za makampuni ambayo yalisajiliwa kwenye mfumo wa zamani na kuyahuisha na kuyapeleka kwenye mfumo wa Usajili kwa njia ya Matandao.

Bw. Mashika aliongeza kwamba kwa kupitia maonesho hayo, BRELA inashauri washiriki na wananchi wote wa jiji la Tanga na maeneo mengine jirani kujitokeza kwa wingi ili kupata huduma hizo muhimu kwa maendeleo ya biashara.

"Sisi BRELA ni taasisi iliyo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara na moja kati ya majukumu yetu ni kutoa elimu kwa wafanyabiashara na wajasiriamali ili wajue namna ya kufuata sheria za kibiashara," alifafanua Bw. Mashika.

Inaendela uk 5

Alisema kwa sasa wafanyabiashara na wajasiriamali hawana sababu ya kuhangaika kwa sababu huduma zao zote zinapatikana kwa njia ya mitandao kupitia tovuti ya BRELA.

“Tunawashauri wafanyabiashara na wajasiriamali kutembelea tovuti yetu ambayo ni rafiki na kufanya maombi yao au kupiga simu namba maalum ya kituo cha miito ili kupata maelekezo endapo watakumbana na changamoto yoyote.”alieleza Bw. Mashika.

Bw. Mashika alisema watu wengi walikuwa na changamoto ya utumiaji wa mifumo kwa njia ya mtandao lakini wamepatiwa usaidizi il kufanikisha upatikanaji wa huduma wanazozihitaji.

Akizungumzia changamoto alisema kuna baadhi ya watu wanaojita wakala wa BRELA maarufu kama "vishoka" ambao hupotosha watu kuwa wanafanya kazi za BRELA wakati siyo kweli.

"Kutokana na hali hiyo kuna baadhi ya wafanyabiashara ambao hudanganywa na hivyo kusajiliwa kwa vyeti vya kughushi. Tumewafuatilia wafanyabiashara hao na kuwapa vyeti halisi wakati tukiendelea na ufuatiaji wa watu hao walioghushi vyeti na saini za maofisa wetu ili waweze kuchukuliwa hatua za kisheria,” Bw. Mashika alibainisha.

# Mwambe akunwa na utendaji wa BRELA



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayesimamia Uwekezaji, Geofrey Mwambe.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayesimamia Uwekezaji, Mhe. Geofrey Mwambe, ameeleza kuridhishwa kwake na utendaji wa BRELA, hasa katika azma ya kuwafikia wadau wake popote walipo.

Mhe. Mwambe alitoa kauli hiyo wakati wa ufunguzi wa Tamasha la kuamasisha Utali na Maonesho ya Biashara yaliyofanyika Wilayani chato mkoani Geita tarehe 7-15 Agosti, 2021.

Waziri Mwambe,ambaye alikuwa mgeni rasmi katika ufunguzi watamasha hilo, baada ya kupata Maelezo kuhusu huduma za papo

Na: Nehemia Mihayo



*Afisa Biashara Bw. Paul Peter (kushoto) akitoa elimu kuhusu huduma zinazotolewa na na BRELA kwa Wanafunzi kutoka Shule ya Sekondari Jikomboe iliyopo Chato, Geita walipofika katika banda la taasisi hiyo kwenye Tamasha la kuhamasisha Utalii na Maonesho ya biashara.*

kwa papo zilizokuwa zinatolewa na BRELA katika maonesho hayo, alieleza kuridhishwa kwake na kuitaka BRELA kuwafikia wafanyabiashara katika maeneo yao ili waweze kusajili biashara zao.

Afisa Msaidizi wa Usajili wa BRELA, Bw. Seleman Seleman, alisema kwamba ushiriki wa taasisi yake katika maonesho ya Geita ilikuwa ni sehemu ya jitihada za kuwafikia wafanyabiashara katika maeneo yao na kuwatatulia changamoto zinazowakabili.“Hivi sasa mtu yeyote anayehitaji huduma zetu hana haja ya kusafiri kuja ofisini.

"Usajili unafanyika kwa njia ya mtandao ukiwa mahali popote na muda wowote. Licha ya kutoa huduma kwa njia ya mtandao, tumechukua hatua zaidi kuwafuata wafanyabiashara katika maeneo yao na kuwapa huduma. Tunakutana nao na kuwatatulia changamoto zao papo kwa papo,” Bw. Seleman alisema.

Aliongeza kuwa wakazi wa Mkoa wa Geita na mikoa jirani watumie fursa hiyo kufika katika maonesho hayo ili waweze kupata elimu na huduma kwa haraka.

Washiriki wa Tamasha hilo waliipongeza BRELA kwa huduma zake kwa wananchi.

Haliswa Chobba, mfanyabiashara na mshiriki wa maonesho hayo kutoka jijini Dar es Salaam aliyefanikiwa kusajili jina la biashara yake papo kwa papo, alisema amefurahishwa na huduma za BRELA baada kupata cheti chake papo kwa papo.

Naye Bw. Jovin Mwarabu, aliyefanikiwa kupata huduma ya kulipia Mizania ya Mwaka (Annual returns), alisema huduma za BRELA zitawahamasisha watu wengi kufanya usajili, hasa wale wasiokuwa na uelewa mpana wa matumizi ya mitandao.

Katika maonesho hayo ili kufanya usajili wa papo kwa papo, wadau walitakiwa kuwa na namba ya Kitambulisho cha Taifa na barua pepe inayofanya kazi.

Kwa watu waliotuma maombi ya huduma mbalimbali ambayo hayajakamilika, walihimizwa kufika banda la BRELA kupata maelekezo ili kukamilisha maombi yao.

BRELA
WAKALA YA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI

***"Tunaipa utu wa kisheria Biashara yako"***

# Tanzania kunufaika na Haki Miliki



*Balozi wa Tanzania nchini Uganda Dkt. Aziz Polnary Mlima (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na wajumbe wa mkutano mkuu wa Shirika la Haki miliki la Afrika (ARIPO) kutoka Tanzania wakiongozwa na Waziri wa Viwanda na Biashara Prof. Kitila Mkumbo (watatu kutoka kulia), Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Pauline Gekul ( wanne kutoka kulia) na Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa (kulia), mara baada ya kusainiwa kwa itifaki ya Haki Miliki jijini Kampala, Uganda Agosti 27, 2021*

**Na: Roida Andusamile**

Nchi wanachama wa Shirika la Kanda ya Afrika la Miliki Ubunifu (Africa Regionl intellectual Property- ARIPO) wamekutana Kampala, Uganda kujadili masuala ya Miliki bunifu Kanda ya Afrika.

Mkutano huo mkuu wa siku tisa ulifunguliwa na Mwanasheria Mkuu wa Uganda, Mheshimiwa Kiryowa Kiwanuka, katika hoteli ya Munyonyo jijini Kampala.

Mgeni rasmi alisisitiza ushiriki wa nchi wanachama kujadili kwa kina itifaki ya ulinzi wa hiari wa Haki Miliki ili kuongeza tija na ufanisi kwa nchi wanachama kwenye kulinda wasanii na kazi zao.

Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) Bw. Godfrey Nyaisa ambaye alishiriki katika mkutano huo alisema washiriki walijadili na kupitisha Itifaki hiyo na kisha kuridhiwa na Mawaziri wa nchi wanachama.

"Kwa upande wa Tanzania, utiaji saini wa Itifaki hii utasaidia wasanii kusajili na kupata ulinzi wa kazi zao nje ya nchi wanachama, ambapo ni tofauti na ilivyo sasa msanii akisajili ARIPO anaweza kuomba ulinzi nchi mbalimbali", alieleza Bw. Nyaisa.

Bw. Nyaisa aliongeza

Inaendela uk 8

kwa kusema kuwa Itifaki hiyo ya Usajili na Ulinzi wa Hiari ya Miliki Bunifu ilisainiwa na Mawaziri wa nchi wanachama wa ARIPO tarehe 27 Agosti, 2021 baada ya kuijadili kwa kina. BRELA ni taasisi inayosimamia masuala ya Miliki Ubunifu ambayo ni nyanja inayohusu uwezo wa ubunifu wa mtu au watu katika kuunda vitu au kutoa huduma. Inahusisha masuala ya hataza, tunzi, fasihi na kazi za sanaa, alama kwenye bidhaa na huduma, maumbo ya mikebe ya bidhaa na nyinginezo.

Pia inahusu uwezo wa ubunifu wa binadamu unaotambuliwa chini ya mfumo wa Sheria wa Ulinzi wa bunifu mbalimbali. Mbali ya ushiriki wa BRELA washiriki wengine kutoka Tanzania walikuwa ni Wizara ya Viwanda na Biashara na Chama cha HakiMiliki Tanzania (COSOTA).

# BRELA yatakiwa kuwatafuta wavumbuzi, wabunifu Tanzania

Na: Nehemia Mihayo

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imetakiwa kubuni mkakati wa kuwafikia wagunduzi na wabunifu ili kusajili shughuli zao. Wito huo ulitolewa na aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Morogoro Bw. Bakari Msulwa Aprili mwaka huu, wakati akifungua zoezi la siku mbili la kutoa elimu kwa wakazi wa Mkoa Morogoro kuhusu huduma zinazotolewa na BRELA katika tukio lililofanyika Ukumbi wa Midland Inn Hotel mjini Morogoro.

Alisema kwamba kwa kuwa kuna Watanzania wengi wanaofanya juhudi za kugundua vitu vipya ni vema BRELA ikabuni mpango wa kuwafikia na kuwasaidia katika masuala ya kurasimishwa kazi zao. Wafanyabiashara wa Mkoa wa Morogoro waliishukuru BRELA kwa kutoa elimu katika mkoa wao ambayo imewapa mwanga na dira mpya katika urasimishaji wa biashara zao.




*Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Mhe. Bakari Msulwa akifungua zoezi la siku mbili la kutoa elimu kwa wakazi wa mkoa huo kuhusu huduma zinazotolewa na BRELA katika ukumbi wa Midland Inn Hotel, mkoani Morogoro, Aprili 21, 2021*

Mfanyabiashara Bi Paulina Mbawala alisema kwamba kabla ya mafunzo hayo kuna vitu vingi walikuwa hawavijui na hivyo kupata ugumu katika kurasimisha biashara zao.

"Kabla ya mafunzo haya hatua za usajili wa kiwanda tuliziona ni ngumu. Lakini kwa kupitia elimu tuliyopata hapa tumefahamu namna gani tunaweza kurasimisha biashara zetu na jinsi ya kukuza biashara kutoka hatua moja kwenda nyingine kwa manufaa yetu wajasiriamali na taifa kwa ujumla," alisema Bi. Mbawala.

Mfanyabiashara mwingine aliyeshirki mafunzo hayo, Bw. Novatus John, alibainisha kuwa kwa sasa wamefahamu ni jinsi gani wanaweza kuingia katika fursa nyingine ili kukuza biashara.

"Kupitia elimu hii tumeweza kufahamu namna ya kupata

Inaendela uk 9

masoko, kuzitambulisha bidhaa zetu sokoni, lakini pia kupitia Dirisha la Taifa la Biashara (The Tanzania National Business Portal) tumejifunza kuwa mfanyabiashara anaweza kufahamu taratibu za usafirishaji nje ya nchi, uingizaji na upitishaji wa mazao na bidhaa mbalimbali nchini," alisema Bw. John Akizungumza na waandishi wa habari katika ufunguzi wa mafunzo hayo, Afisa Leseni Mwandamizi wa BRELA, Bw. Abbas Cothema, alisema sehemu walizopita kutoa mafunzo wamegundua kwamba wafanyabishara wamekuwa wakitumia majina ya biashara kabla ya kuyasajili na badaye yakaleta shida katika usajili.

"Mpaka sasa tumetoa elimu kwa wafanyabiashara wa Mkoa wa Singida, Dodoma na sasa tupo hapa Morogoro changamoto inayojirudia ni kufanya biashara bila kurasimisha," alisema Bw. Cothema.

Aliongeza kuwa mfanyabiashara anaanzisha biashara leo halafu anakuja kusajili miaka mitano badaye. Kwa wakati huo kama alikuwa anatumia jina la biashara lisilosajiliwa itamlazimu kulibadili na kuanza kujitangaza upya.

# Aipongeza BRELA kutoa elimu kwa umma




*Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dkt. Rehema Nchimbi (katikati) akitoa hotuba ya ufunguzi wa semina ya utoaji elimu kuhusu usajili na Leseni iliyofanyika katika Ukumbi wa Roman Catholic tarehe 13 Aprili, 2021*

**Na: Nehemia Mihayo**

Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dkt. Rehema Nchimbi, ameipongeza Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni BRELA kwa kuelimisha umma kuhusu huduma zinazotolewa na taasisi hiyo.

Alitoa pongezi hizo mapema Aprili mwaka huu wakati akifungua semina ya siku mbili ya huduma ya elimu kwa umma iliyoandaliwa mahsusi kwa wakazi wa Singida.

Alisema kwamba alifurahishwa na ujio wa BRELA mkoani humo kwa kuwa itakuwa ni hamasa kubwa kwa wajasiriamali kurasimisha biashara zao.

"Kuna elimu nyingi zinazotolewa, lakini elimu ya BRELA ina thamani kubwa kwa maendeleo ya Taifa letu. Niliposikia mnakuja mkoani Singida nilifurahi sana kwa kuwa badala ya wananchi kuwafuata, ninyi ndiyo mmewafuata ," alisema Dkt. Nchimbi.

Mkuu huyo wa mkoa mstaafu alisema kuwa Singida ya sasa siyo ile ya zamani kwa sababu leo zipo fursa nyingi za uwekezaji na idadi ya wafanyabiashara na wajasiriamali imekuwa ikiongezeka siku hadi siku.

"Singida kwa miaka mingi imekuwa ikionekana siyo mkoa wa kibiashara, lakini leo nimefarijika sana kuona kwamba mmefika katika mkoa huu. Hii inamaanisha mmeona kwamba wapo wafanyabiashara na wajasiriamali wa kutosha," alisema Dkt. Nchimbi.

Naye Afisa Leseni Mwandamizi wa BRELA, Bw. Abbas Cothema, alibainisha kwamba kwa mwaka 2020/21 Taasisi iliweka mikakati kadhaa, mmojawapo ikiwa ni kutoa elimu kwa umma kuhusu majukumu yake ambayo ndiyo inatekeleza kwa sasa.

# BRELA yawafariji wagonjwa Dar

Na. Christina Njovu

Wakala wa Usajili wa Biashara na Lesini( BRELA) imeadhimisha wiki ya Utumishi kwa Umma kwa kutembelea wagonjwa Hospitalini, Kufanya Usafi a kutoa elimu ya huduma za Usajili wa Biashara na Leseni kwa wafanyabiashara katika soko la Kisutu, jijini Dar Es Salam

Hatua hiyo ilifikiwa ikiwa ni mwendelezo wa maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma ambayo ilianza Juni 16,2021 na kilele chake kufikia Juni 23,2021, ambapo Wizara na taasisi zake zilitakiwa kutoa huduma kwa wadau wake na wananchi kwa ujumla kutokana na michango wanayoitoa kwa Serikali yao.

Wakiwa katika hospitali ya Amana, Watumishi wa BRELA walikabidhi mahitaji mbalimbali ya wagonjwa ikiwa ni pamoja na Sabuni, Taulo za Kike (Pads) na *Daipers* za watoto na wakubwa. Pia walitumia fursa hiyo kuchangia damu.

Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano kutoka BRELA, Bi. Roida Andusamile akizungumza wakati wa kukabidhi bidhaa hizo alisema Taasisi hiyo pamoja wa kuwezesha biashara kwa kusajili Majina ya Biashara, Kampuni, Alama za Biashara na Huduma, utoaji wa Leseni za Biashara kundi A na Leseni za Viwanda na



*Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano kutoka Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) Bi.Roida Andusamile akitoa maelezo kuhusu misaada mbalimbali iliyotolewa na Taasisi hiyo katika hospitali ya Amana Juni 23, 2021 ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma.*

Hataza, inajali jamii inayoizunguka kwa kuwapatia misaada pindi fursa inapopatikana.

"BRELA imefika hospitali ya Amana na kuchangia mahitaji ya msingi ya wazazi na watoto ili wanapoendelea na matibabu wawe katika hali ya usafi," alifafanua Bi. Andusamile na kuongeza kuwa utaratibu huu utaendelea kufanyika katika hospitali mbalimbali za hapa nchini.

Akipokea msaada huo, Daktari Bingwa wa magonjwa ya kinamama Dkt. Baya Kissiwa aliishukuru BRELA kwa msaada wake kwa wagonjwa na kutoa wito kwa taasisi nyingine kufika hospitalini hapo na kuwasaidia wagonjwa.

Dkt. Baya alisema kuwa hospitali hiyo kwa sasa ina uhitaji mkubwa wa damu hasa kwa wazazi wanaofika hospitalini hapo kwa matibabu, hivyo inawaomba wananchi kuchangia damu ili kuokoa maisha ya mama na mtoto.


Aidha katika soko la Kisutu, watumishi wa BRELA walitoa elimu kwa wafanyabiashara na kuwahimiza kurasimisha biashara ili kuzipa utu wa kisheria.

Pamoja na kutoa elimu sokoni hapo, Watumishi wa BRELA walifanya usafi ndani ya soko hilo, ikiwa ni moja ya jukumu la watumishi wa umma

Inaendela uk 11

kuwajibika kwa wananchi. Awali Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA Bw. Seka Kasera alitumia Wiki ya Utumishi wa Umma kwa kuwahudumia wateja waliofika katika ofisi za BRELA kupata huduma mbalimbali. Maadhimisho haya yanaoyoratibiwa na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora yalifanyika sambamba na kaulimbiu isemayo "Kujenga Afrika tunayoitaka, kupitia utamaduni wa uadilifu ambao unastawisha uongozi wenye maono hata katika mazingira ya mgogoro."

# Dodoma watakiwa kuchangamkia elimu ya BRELA



*Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dkt. Binilith Mahenge (wa tano kutoka kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya washiriki wa mafunzo ya siku mbili kuhusu huduma zinazotolewa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) kwa wakazi wa Dodoma yaliyofanyika katika ukumbi wa mkutano uliopo Makao Makuu ya Jeshi la Zimamoto, Jijini Dodoma Aprili 17, 2021.*

**Na: Nehemia Mihayo**


Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dkt. Binilith Mahenge, amewataka wananchi wa mkoa huo kuchangamkia elimu inayotolewa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) katika kujikwamua kiuchumi.

Dkt. Mahenge ambaye hivi sasa ni Mkuu wa Mkoa wa Singida, akifungua mafunzo ya siku mbili kwa wakazi wa Dodoma katikati ya mwezi Aprili 20121 mwaka huu kwenye Ukumbi wa Mikutano Makao Makuu ya Jeshi la Zimamoto, aliwaambia washiriki kwamba kufanikiwa katika biashara ni vyema biashara au shughuli husika irasimishwe na kutambulika kisheria.

"Hatua ya kwanza ya kufanikiwa katika biashara hiyo kuirasimisha biashara na ikiwa inatambulike kwa mujibu wa sheria. BRELA wapo hapa Dodoma kwa siku mbili kwa hiyo hii ni fursa kubwa na adhimu,"alisisitiza Dkt. Mahenge.

Msimamizi wa BRELA, Kanda ya Kati, Bw. Gabriel Girangay, alisema kwamba licha ya elimu hiyo kwa wote inayotolewa kwa siku mbili, ofisi ya BRELA mkoani Dodoma ipo tayari kuwahudumia na inafanya maandalizi ya kufika katika wilaya zote tisa za mkoa wa Dodoma kwa ajili ya kutoa elimu kwa wananchi kuhusu huduma za Taasisi.

# Wafanyabiashara wa mifugo Pugu wanolewa




*Afisa Tehama Msaidizi, Bw. Hillary Mwenda (kulia) kutoka Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) akimkabidhi Leseni ya Biashara kundi A, Bw. Gilbert Chizua mara baada ya usajili wa papo kwa papo katika mafunzo ya Uwezeshaji wa upatikanaji wa Leseni za Biashara katika mnada wa mifugo Pugu jijini Dar es Salaam*

**Na: Sheila Mfunami**

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imetoa mafunzo ya siku saba kwa wafanyabiashara wa mifugo waliopo Pugu mkoani Dar es Salaam kuhusu upataji wa leseni za biashara kwa njia ya mtandao. Mafunzo hayo yalikwenda sambamba na utoaji wa elimu kuhusu umuhimu wa upataji leseni ya biashara, elimu ambayo imekuwa ngumu kwa kundi hilo la wafanyabiashara.

BRELA iliona ipo haja ya kusogeza huduma hizo kwa wafugaji kama ambavyo imekuwa ikifanya kwa wajasiriamali na maonesho mengine mbalimbali ambapo wafanyabiashara wamekuwa wakipata huduma za BRELA papo kwa papo.

Afisa Biashara wa BRELA, Bw. Peter Riwa, ambaye alikuwa akiongoza mafunzo hayo, alieleza lengo kuu la mafunzo hayo ni kutoa elimu na hamasa kwa wafanyabishara wa mifugo ili waweze kurasimisha biashara zao.

Bw. Riwa alisema BRELA imeamua kuwafikia wadau wetu na kuwapa elimu juu ya huduma inazotoa ambazo ni pamoja na Usajili wa Kampuni, Usajili wa Jina la Biashara, Usajili wa Alama ya biashara na huduma, utoaji wa Leseni za Biashara kundi A, utoaji wa Leseni za Viwanda pamoja na Hataza.

Huduma nyingine ni pamoja na za baada ya usajili na kupata Leseni na kupata taarifa kwa njia ya mtandao sambamba na kuwahamasisha wadau juu ya upatikanaji wa Leseni za biashara.

Vile vile kuwasogezea huduma karibu na kutatua changamoto za wadau papo kwa papo pindi wanapopatiwa elimu.

Uendeshwaji wa zoezi hilo ni mkakati wa BRELA katika kuondoa na kupunguza urasimu wa uwepo wa watu wa kati maarufu kwa jina la VISHOKA ambao wamekuwa wakikwamisha taratibu za upatikanaji wa leseni kwa wafanyabiashara, alieleza Bw. Riwa.

Mkuu wa mnada wa ng'ombe wa Pugu, Bw. Kerambo Samwel, alifurahishwa na hatua iliyochukuliwa na BRELA ya kuwafikia wafanyabiashara wa mifugo mahali walipo, hasa katika eneo hilo na kuongeza kuwa hii itawawezesha wafanyabiashara hao wa mifugo kupata leseni za biashara kwa urahisi.

"Nawapongeza BRELA kwa juhudi kubwa amabazo mnazifanya ."alifafanua Bw. kerambo.

Licha ya pongezi hizo, Bw. Kerambo alieleza changamoto ambazo wafanyabiashara wa mifugo wamekuwa wakikumbana nazo, ikiwemo kufanya biashara bila leseni. Hali hiyo inawafanya wafanyabiashara kutumia Leseni moja zaidi ya mtu mmoja, jambo ambalo ni kinyume cha sheria.

Baadhi ya

Inaendela uk 13

wafanyabiashara hao walieleza kuwa wamekuwa wakirithi biashara ya mifugo kutoka kwa wazazi wao hivyo kufanya biashara hiyo kwa mazoea.

Wafanyabiashara hao wamekuwa wakishindwa kufuatilia Leseni zao kwa kuogopa makadirio ya kodi.

Wakati wa mafunzo hayo wafanyabiashara 22 walijitokeza kurasimisha biashara zao na kupata leseni huku wakiiomba BRELA kuwa na tawi mnadani .

# BRELA yawapa somo Wabunifu kusajili vumbuzi

**Na. Christina njovu**

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imewapa mafunzo wabunifu walioshiriki mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) yaliyofanyika katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

Akizungumza katika mafunzo hayo yaliyofanyika tarehe 6-11 Mei 2021 Jijini Dodoma, Afisa Utumishi na Utawala anayehusika na Uchambuzi wa Hataza na Alama za Biashara Bw. Raphael Mtalima alisema; mvumbuzi lazima alinde Ubunifu wake kisheria.

“Tuko hapa kutoa elimu kwa wabunifu wetu 70 ambao wameingia kwenye Mashindano ya Sayansi Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) mwaka huu, lengo ni kutaka wabunifu walinde bunifu zao kisheria,” alisema Bw. Mtalima.

Mtalima alisema wabunifu wamekuwa wakitumia gharama kubwa kutengeneza




*Afisa Mwandamizi Utumishi na Utawala wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Raphael Mtalima akitoa mada juu ya sifa za Uvumbuzi unaoweza kusajiliwa na Wakala katika semina ya Wabunifu katika Mashindano ya Sayansi Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) yaliyofanyika Jijini Dodoma kuanzia tarehe 6 hadi tarehe 11 Mei,2021.*

bunifu zao hivyo wana kila sababu ya kulinda bidhaa zao kisheria kwa kusajili bunifu zao BRELA.

“Kuna watu wapo kwa ajili ya kuangalia nani kafanya nini,akiona kitu kimebuniwa kizuri, hunakili na kujimilikisha kisheria kwa kufanya Usajili na kuwa na hakimiliki,” alisema Afisa huyo.

Aidha Mtalima aliwaeleza kuwa wabunifu hao wakisajili Bunifu zao zitawasaidia katika Mambo mengi ndani na nje ya nchi ikiwa ni pamoja na kutambulika popote.

Mmoja wa Wabunifu waliokuwepokatikamafunzo hayo Bw. Emmanuel Matola; ambaye amebuni mfumo rahisi wa kufundishia

Inaendela uk 14

ufundi wa magari alisema, mafunzo hayo waliyopata yatawasaidia kupata Ulinzi wa bidhaa zao.

"Unajua wabunifu wengi wa hapa nchini hawana utamaduni wa kusajili bunifu zao BRELA ,hivyo Mara nyingi hujikuta wakikosa haki zao inapotokea mtu kaiba ubunifu wa mtu mwingine," alisema Bw. Matola.

Naye Bi. Martha Machumu ambaye ni mbunifu mwanafunzi wa Kidato cha Sita katika Shule ya Sekondari Nganza iliyopo Jijini Mwanza alisema amefurahi kupata elimu hiyo ambayo anaamini itamsaidia katika shughuli zake za kibunifu.



*Baadhi ya Wabunifu wakifuatilia mafunzo yaliyotolewa na Afisa Mwandamizi- Utumishi na Utawala kutoka Idara ya Miliki Ubunifu BRELA, Bw. Raphael Mtalima (hayupo pichani) kuhusu sifa za Uvumbuzi zinazoweza kusajiliwa kama Hataza wakati wasemina iliyofanyika Dodoma tarehe 6 hadi 11 Mei, 2021.*

***"Rasimisha Biashara yako kwa maendeleo ili kuinua uchumi wa taifa"***

# Mchango wa Jina la Biashara katika soko la ushindani

Katika biashara, ni vigumu kuepuka ushindani. Hii ni kwa sababu katika biashara yeyote mtu atakayoanzisha ni lazima kuna watangulizi katika biashara hiyo.

Pia, kuna watu wengine watakaokuja baada ya kupenda biashara hiyo.

Kwa mjasiriamali au mfanyabiashara yeyote ni vyema kufahamu bayana kwamba ili biashara ikue, ni lazima wigo wake katika soko uongezeke kwa kadri muda unavyokwenda. Wigo wa soko hupimwa kwa kuangalia biashara inayotoa huduma au kuuza bidhaa zake kwa kiwango kikubwa kushinda biashara nyingine za namna moja.

Kwa mfano, kama soko la uuzaji maji ni asilimia mia moja na wafanyabiashara katika soko hilo wapo watatu -- yaani A, B na C -- mfanyabiashara A ameshika soko kwa asilimia 40 huku wafanyabiashara B na C wakishika kwa asilimia thelathini kila moja. Kwa hali hii, mfanyabiashara A ndiye amelishika soko hilo kwa sehemu kubwa zaidi. Makala hii inachambua mikakati kadhaa ambayo mfanyabiashara anaweza kuitumia ili kujiongezea nafasi katika soko la bidhaa anayouza au huduma anayotoa.

## UBUNIFU

Mmoja wa wataalam wa masuala ya masoko, Leslie Kramer, anaeleza kwamba ili mfanyabiashara apate

Inaendela uk 15

nafasi katika soko, ni lazima awe mbunifu katika njia za kufikisha bidhaa au huduma zake kwa wateja wapya. Ubunifu huu pia ni kutumia mbinu katika biashara yake ambazo hazijawahi kutumiwa na wapinzani katika soko hilo.

### MTEJA NI MFALME

Siri moja ya biashara ni kuhakikisha idadi ya wateja haipungui; mfanyabiashara mzuri hujenga uhusiano mzuri na wateja wake ili wasihamie kwa mfanyabiashara mwingine.

Wahenga walisema mteja ni mfalme; anapenda siku zote kusikilizwa na kupewa huduma ya kumridhisha.

Hivyo mfanyabiashara unatakiwa kujenga uhusiano mazuri na wateja kwa kuwasikiliza na kufanyia kazi maoni yao.

Jitihada hizi zinatakiwa ziende sambamba na kuvutia wateja wapya. Kwa kufanya hivyo, tarajia matokeo mawili: moja ni yako na mbili utavutia wateja wapya kila siku, na hivyo kuendeleza biashara.

### TENGENEZA MKAKATI WA KUONGEZA WIGO WA SOKO

Mkakati huu unasimamia vitu viwili vikuu: malengo na muda wa kuyafikia. Unaweza kuwa wa mwaka mmoja na ukagawa utekelezaji wake kwa awamu nne, kila awamu ikiwa na miezi mitatu.

Mkakati huu utasaidia kupima na kufahamu kama malengo uliyoweka kutekeleza katika kila awamu umefanikiwa au hapana na pia kujua sababu.

### KUIPATIA JINA BIASHARA YAKO

Jina la Biashara ni utambulisho wa biashara fulani. Jina hili huipatia biashara uwezo wa kutambulika na kukumbukwa na wateja katika namna mbalimbali.

Wateja wanaweza kuitambua biashara yako kwa kutajiwa jina pekee, hata kama hawajawahi kufika; lakini pia wanaweza kuitambua biashara kwa kuelekezwa na watu wengine na wakafika sehemu ilipo biashara hiyo.

Jina la Biashara pia ni muhimu kwa ajili ya kuitangaza biashara yako kupitia njia mbalimbali na watu wakaifikia kwa urahisi.

Ni muhimu pia kuzingatia kwamba Jina la Biashara lina sifa kuu ya upekee; halitakiwi kufanana na jina la mtu mwingine kwa sababu hii itawachanganya wateja kwa kiasi kikubwa ambao watahitaji huduma au bidhaa. Mara baada ya kupata Jina la Biashara, namna nzuri ya kulinda upekee ni kufanya usajili katika mamlaka husika ili kupewa haki ya kutumia jina hilo katika biashara peke yako.

Kwa Tanzania, mamlaka inayohusika na Usajili wa Jina la Biashara BRELA, ambayo inatoa huduma hii kwa njia ya mtandao. Kigezo pekee kwa ajili ya kusajili Jina la Biashara ni kuwa na namba ya kitambulisho cha taifa kutoka NIDA.

Pia anayehitaji kusajili Jina la Biashara atatakiwa kufungua akaunti katika Mfumo wa Usajili kwa njia ya Mtandao ya ORS, na hivyo atatembelea tovuti ya www.brela.go.tz na kufungua akaunti hiyo. Baada ya kufungua akaunti, atatakiwa kuandaa ombi lenye taarifa zake za biashara na kutuma BRELA ambapo atalipia kiasi cha Sh. 20,000/-. Kisha atapata cheti ambacho kinampatia haki ya umiliki wa jina hilo la biashara. Wahenga walisema “motto umleavyo ndivyo akuavyo.” Kwa usemi huu biashara ni kama mtoto, njia ambazo zinatumika kuilea ndizo zitakazoifanya ikue, idumae au ifilisike.

**Na: Nehemia Mihayo**

# Sababu 5 muhimu za kusajili Alama ya Biashara

Alama ya Biashara au huduma ambayo kwa wengi hujulikana kama nembo au 'logo' ni alama pekee inayotambulisha aina fulani ya bidhaa au huduma inayotolewa au kuzalishwa na mtu, kikundi au kampuni fulani.

Kihistoria, Usajili wa Alama hizi ulianza kufanyika chini ya sheria karne ya 19 ingawa ni bayana kwamba hata kabla ya hapo alama hizi zilikuwa zikitumika.

Moja ya sababu kubwa ya kuanza kusajili Alama za Biashara au huduma ni ukuaji wa teknolojia, hasa kuongezeka kwa masafa ya vyombo vya habari katika kuwafikia watu wengi zaidi. Alama za mwanzo kusajiliwa ni pamoja na 'Deviled Entremets' iliyosajiliwa mwaka 1870 na Kampuni ya William Underwood huko Boston, Marekani.

Mwaka 1875, mfanyabiashara William Bass aliingia katika historia ya kusajili Alama ya Biashara ya kwanza nchini Uingereza iliyojulikana kama 'Red Bass triangle'.

Alama hii ilikuwa na mwonekano wa pembe tatu nyekundu (kitako kikiwa chini na ncha kali ikiangalia juu), na maneno yaliyosomeka Bass.

Nchini China Alama ya kwanza kusajiliwa ilijulikana kama 'Nestle Eagle Brand' ambayo ilisajiliwa 1874. Hizo ni baadhi ya Alama za kwanza kusajiliwa katika nchi mbalimbali.

Kwa Tanzania alama ya biashara ya kwanza kusajiliwa ilijulikana kama 'His maters Voice' iliyosajiliwa Septemba 11, 1922.

Kila jambo linalofanyika kuna sababu kadhaa nyuma yake, vivyo hivyo kwa usajili wa Alama hizi. Makala hii inachambua sababu tano muhimu za kusajili Alama za Biashara au Nembo"."

### UTAMBUZI WA BIDHAA/ HUDUMA

Sifa kuu ya Alama ya Biashara au Huduma ni kutofautisha bidhaa moja kati ya nyingine zinazofanana. Kwa mfano, bidhaa ya maji ya chupa ya kunywa zote ni bidhaa ila zinatofautishwa na alama ya bidhaa au Nembo. Kwa bidhaa za aina moja ziingiapo sokoni ni vigumu sana kutambua utofauti zake, hivyo kumfanya mnunuzi kushindwa kuwa na uhakika na bidhaa atakayonunua.

Hii inaweza kumfanya mteja kushindwa kuitambua pia bidhaa aliyotumia awali atakapohitaji kuitumia tena. Matokeo yake ni kuanza kubahatisha.

Kwa kutumia Alama ya Biashara mteja anaweza kuitambua bidhaa aliyotumia mara ya kwanza kwa kuangalia alama ya bidhaa iliyopo na kuinunua tena.

### KUTANGAZA BIDHAA/ HUDUMA

Alama za Biashara au huduma zina mchango mkubwa katika kuitagaza biashara au huduma fulani, hasa katika matangazo ya michoro na maandishi lakini pia kwa matangazo mengine ambayo huwa siyo ya moja kwa moja. Matangazo haya mara nyingi hujitokeza katika filamu, mabango, vipeperushi, au nyimbo.

Mara kadhaa unaweza kuwa umeshuhudia nembo fulani inajitokeza katika nyimbo au filamu, mathalani katika kinywaji au duka. Hii ni aina fulani ya kutangaza biashara.

Hivyo kuwa na nembo ambayo imesajiliwa

Inaendela uk 17

inaweza kusaidia kwa kiasi kikubwa katika kuifanya bidhaa au huduma iweze kufahamika kwa umma.

### KUFIKA SEHEMU YA BIASHARA/HUDUMA

Siku zote katika maeneo ya biashara, kuna msongamano wa biashara za aina moja. Kwa hali hii, wakati mwingine inakuwa vigumu kwa wateja kutambua sehemu ya biashara ambayo wanakwenda.

Katika mazingira haya, pale nembo inapotumika humsaidia mteja kutambua sehemu ya biashara anayokwenda na kufika kwa urahisi. Hii kwa kiasi kikubwa inasaidia kuongeza idadi ya wateja wanaofika katika eneo lako.

### KUIPA HADHI BIASHARA/ HUDUMA

Katika kutoa huduma au kuuza bidhaa, wateja hugawanywa katika makundi mbalimbali kulingana na mpango wa mauzo wa mtu au kampuni husika.

Mara nyingi kuna baadhi ya wateja kabla ya kununua bidhaa au kupata huduma wanaangalia hadhi ya bidhaa au huduma na mara nyingi kuna baadhi ya watu hawawezi kabisa kununua au kutumia bidhaa za aina Fulani kwa sababu ya hadhi yake.

Katika hali hii nembo ina mchango mkubwa sana katika kuipa hadhi na mwonekano wa kipekee bidhaa au huduma inayotolewa. Pia inamwezesha mteja kufanya maamuzi sahihi kulingana na ubora ya bidhaa au huduma fulani inayotambulishwa na nembo.

### KINGA YA KISHERIA DHIDI YA BIASHARA YAKO

Ni muhimu kuilinda kisheria biashara yako dhidi ya washindani au waharibifu wa biashara za wengine. Mara kadhaa imejitokeza kwamba mtu au kikundi cha watu wanazalisha bidhaa zenye ubora hafifu kwa kutumia nembo ya bidhaa nyingine au kutoa huduma hafifu kwa nembo ya sifa na hadhi sehemu fulani.

Pindi bidhaa hizi ziingiapo sokoni, huharibu sifa nzuri ya bidhaa iliyokuwepo awali. Lakini kama nembo yako ya bidhaa au huduma imelindwa, basi inakuwa ni vigumu kwa watu wengine kutumia nembo hiyo.

Kwa upande mwingine, kuendesha biashara kwa kutumia nembo ambayo haijasajiliwa, mshindani anaweza kuisajili nembo hiyo na kuwa yake bila pingamizi kwa sababu nembo hiyo kisheria haina mmiliki. Endapo mtu atatumia nembo iliyosajiliwa kisheria basi mmiliki anaweza kumchukulia hatua za kisheria kwa kwenda mahakamani kudai fidia ya matumizi yasiyo halali ya nembo yake na hasara aliyopata kwa udanganyifu huo.

### JE UNAWEZAJE KUSAJILI ALAMA YAKO YA BIASHARA AU HUDUMA?

Kwa Tanzania Alama ya Biashara au Huduma (Nembo) zinasajiliwa na BRELA chini ya Sheria ya Alama za Biashara na Huduma Sura ya 326. Taratibu zote za Usajili zinafanyika kwa njia ya Mtandao kupitia tovuti ya www.brela.go.tz. Hakuna haja ya kufika katika Ofisi za BRELA kwa ajili ya Usajili. Ili kukamilisha usajili, mwombaji atatakiwa kuwa na namba ya Kitambulisho cha Taifa cha NIDA ambayo itakayo mwezesha kufungua akaunti katika mfumo wa usajili na kisha kuandaa ombi la usajili na kuliwasilisha BRELA kwa njia ya mtandao.

Jumla ya gharama kwa ajili ya usajili ni Sh. 130,000 zinazolipwa kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza mwombaji atalipa Sh. 65,000 ambayo ni ada ya ombi pamoja na kutangaza nembo kwa umma ili kujiridhisha kama nembo hiyo haina mmiliki mwingine. Awamu ya pili mwombaji

Inaendela uk 18

atalipia Sh. 65,000 ambayo ni ada kwa ajili ya cheti cha usajili baada ya ombi la usajili kukamilika. Muda wa usajili wa nembo ni miezi mitatu ambapo mwombaji atapata cheti cha usajili na kuimiliki nembo yake kisheria.

Katika hiyo miezi mitatu ya usajili kuna takwa la kisheria la kutangaza kwa siku 60 nembo hiyo kwenye jarida la BRELA linalotoka bure kila mwezi. Jarida hilo linapatikana kwenye tovuti ya BRELA. Kisheria alama ya biashara au huduma, ukomo wake ni pale mmiliki wa alama au nembo hiyo atakapoamua kuacha kuitumia kwa kuitaarifu BRELA kupitia kwa Msajili wa Alama za Biashara na Huduma. Sheria ina takwa la kuhuisha nembo hiyo kwa mara ya kwanza baada ya miaka saba na baada ya hapo itakuwa kwa kipindi cha kila baada ya miaka kumi.

Alama ya Biashara na Huduma (nembo) ni mali kama zilivyo mali nyingine na zina thamani kubwa katika biashara. Ni vema wafanyabiashara wa aina zote wakasajili Alama zao za Biashara ili kulinda nembo hizo zisichukuliwe na maharamia wa biashara.

Na: Nehemia Mihayo

# BRELA na mchango wake katika kukuza uchumi wa Tanzania




*Maafisa kutoka Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Bw. Lucas Mafuru (kulia) na Bw. Fransice Filimbi (pili kulia) wakipata maelekezo kutoka kwa Meneja Uzalishaji wa Kiwanda cha Maji cha Dew Drop Drinks Company Limited Bw. Felix kessy(mwenye koti jeupe) kuhusu hatua za uzalishaji. Maafisa hao walifika katika kiwanda hicho kwa ajili ya kufanya ukaguzi na kutoa elimu kuhusu huduma za Usajili na utoaji wa Leseni za Viwanda.*

Inaendelea uk 19

Biashara ni nguzo muhimu kwa maendeleo taifa lolote duniani. Katika nchi ambayo biashara za kila aina zimesimamiwa na kupewa kipaumbele, biashara hizo zimeweza kusaidia kupunguza changamoto za ajira kwa watu wengi.

Biashara ni chanzo cha mapato kwa serikali na kwamba raia wengi wanapowekeza katika biashara serikali inapata mapato faida kupitia kodi, na hivyo kuwekeza katika miradi ya maendeleo na huduma za kijamii.

Biashara pia huboresha mahusiano ya nchi moja na nyingine kutokana na uuzaji wa bidhaa ndani ya nchi na nje. Hii ni kutokana na nchi mbili au zaidi kutegemeana katika upatikanaji wa bidhaa ya aina fulani.

Nchini Tanzania, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), ni lango la kuingilia kwa wafanyabiashara wakubwa na wadogo, wajasiriamali wakubwa na wadogo pamoja na wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi.

Katika jitihada za kuweka mazingira mazuri kwa wadau wake, BRELA imefanya maboresho makubwa kwenye mifumo yake ya kiutendaji.

**Yafuatayo ni baadhi ya maboresho ambayo yamefanyika:-**

### MFUMO WA USAJILI KWA NJIA YA MTANDAO (ORS)

Mwaka 2018, BRELA iliachana rasmi na utaratibu wa utoaji wa huduma kwa njia ya karatasi ngumu na kuanza kutumia mfumo wa usajili kwa njia ya mtandao (Online registration system). Mfumo huu wa usajili ni sehemu ya uboreshaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji. Wafanyabiashara kote nchini sasa wanaweza kurasimisha biashara zao wakiwa popote walipo.

Mfumo huu imepunguza gharama kwa wafanyabiashara ambao hapo awali ilibidi wasafiri kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania kwenda Ofisi Kuu ya BRELA ili kukamilisha usajili wao.

Taarifa iliyotolewa Aprili mwaka huu na Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Godfrey Nyaisa, inasemja kwa mwaka 2020/21 malengo ya usajili yalikuwa ni kusajili kampuni 9,528 ambapo mpaka mwishoni mwa mwezi huo tayari kampuni zilizosajiliwa zilikuwa 7,148, sawa na alisilimia 75.

Mafanikio hayo ni kiashiria kwamba mfumo umekuwa chachu kubwa kuwavutia watu kufanya usajili mbalimbali wakiwa katika maeneo yao ya kazi, nyumbani au mapumzikoni. Hata hivyo, pamoja na mafanikio hayo, baada ya kuutumia mfumo kwa takribani miaka miwili, changamoto kadhaa zimebainika baada ya kupokea maoni na mapendekezo kutoka kwa watumishi wa ndani lakini pia wadau wa BRELA.

Mwezi Mei mwaka jana BRELA kwa kushirikiana na wataalam wa mifumo toka taasisi mbalimbali za serikali ilianza rasmi kubadilisha na kuboresha mfumo (system re-designing) kwa kuzingatia changamoto zilizopo katika mfumo unaotumika hivi sasa.

Kukamilika kwa mfumo huo kutaweza kutatua changamoto zilizopo, ikiwa ni pamoja na maombi kupokelewa na kufanyiwa kazi na ofisa mmoja, ombi kufanyiwa kazi kwa kuzingatia ombi lililotangulia (first come, first served), kuendelea kuunganisha mfumo wa BRELA na mifumo ya taasisi nyingine kama Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Benki, Uhamiaji na Mamlaka za utoaji Leseni katika Halmashauri.

Inaendela uk 20

Lengo kuu ni kutengeneza mazingira rafiki na wezeshi siyo tu kwa wawekezaji bali pia kwa wafanyabiashara wote.

### UANZISHWAJI OFISI YA KANDA YA KATI

Licha ya kutoa huduma zake kwa njia ya mtandao, BRELA imefungua mlango mwingine kwa wafanyabiashara waliopo Kanda ya Kati, mbali na ofisi zingine za kanda ya Ziwa na Kusini zilizofunguliwa awali ili waweze kupata huduma kwa haraka na kuendeleza biashara zao.

Aprili 17 mwaka huu Msimamizi wa Ofisi ya BRELA jijini Dodoma na Kanda ya Kati, Gabriel Girangay, alikaririwa akisema kwamba ofisi imeandaa mkakati mzuri wa kuwahudumia wadau wake, hakuna atakayefika katika ofisi hizo na kuondoka bila ya changamoto zake kutatuliwa.

Girangay pia alibainisha kuwa mpango wa ofisi hiyo kufika katika kila mkoa uliopo Kanda ya Kati na kutoa elimu na usaidizi kwa wadau wake wote, zoezi ambalo litaanzia katika mkoa wa Dodoma.

### UANZISHWAJI WA KITUO CHA MIITO

Katika kuhakikisha kwamba wadau wote wanapata usaidizi wa haraka katika kupata huduma za BRELA, kituo cha miito cha kisasa kilianzishwa ili kuwasaidia wote wanaokwama kwa namna moja au nyingine.

Kituo hiki kimewekewa mitambo ya kisasa ambayo humsadia anayepiga simu kwa ajili ya kupata usaidizi kupokelewa na njia ya simu ambayo ipo wazi ili kuepusha msongamano wa simu nyingi katika njia moja.

Sambamba na hilo, BRELA imeweka utaratibu mzuri kwa wateja kuwawasiliana kwa njia nyingine kama mitandao ya kijamii (Facebook, Instagram, Twitter,) WhatsApp na hata barua pepe.

Mawasiliano kwa njia hii yote hujibiwa kwa siku moja ili mtu anayehitaji kukamilisha usajili wa aina yeyote aweze kutuma maombi yake yafanyiwe kazi na BRELA.

### MUDA WA KUCHAKATA MAOMBI

BRELA inatoa huduma sita ambazo ni Usajili wa Makampuni, Usajili wa Majina ya biashara, Usajili wa Alama za biashara na huduma, Utoaji wa Leseni ya Biashara kundi A, Utoaji wa Leseni ya Kiwanda, Utoaji wa Hataza Huduma hizi zinatofautiana kila moja na muda wake kulingana na matakwa ya sheria ya huduma husika.

Mathalani, muda wa usajili wa jina la biashara ni siku moja na si zaidi ya siku tatu za kazi, usajili wa kampuni ni siku tatu na si zaidi ya siku tano za kazi.

Usajili wa Alama za Biashara na huduma ni kipindi cha siku tisini (kutokana na takwa la kisheria). Maombi ya kupata Hataza ni siku mia moja na ishirini (120) (kutokana na takwa la kisheria), kupata leseni ya kiwanda au leseni ya biashara kundi A ni siku moja na si zaidi ya siku tatu za kazi.

Yote hii ni kuhakikisha kwamba wafanyabiashara wengi zaidi wanapata huduma za BRELA kwa sababu ndiyo lango kuu la Wafanyabiashara, wajasiriamali, wawekezaji na wadau wengine wengi.

### UKARABATI WA OFISI MPYA ZA BRELA

Katika kuhakikisha kwamba huduma bora zinatolewa kwa wadau wake, BRELA imekamilisha ukarabati wa ofisi mpya na kuhamia. Ukarabati wa jengo hili utaongeza nafasi zaidi kwa watumishi wa BRELA, mifumo ya TEHAMA na hivyo kuongeza ufanisi zaidi katika huduma zinazotolewa.

### MAANDALIZI YA TOVUTI MPYA YA BRELA

Pamoja na kuwa na Tovuti inayotumika sasa,

Inaendela uk 21

taasisi tayari inaendelea na maandalizi ya tovuti mpya ambayo itakuwa ni rahisi na itawasaidia Watanzania wote kupata taarifa wanazozihitaji.

Jitihada hizi zinazofanywa na BRELA ni sehemu tu ya mkakati wa taasisi wa kuhakikisha kwamba uchumi wa Tanzania unaimarika kupitia biashara, kuongezeka ajira, kuongezeka pato la taifa kwa mjalipo ya kodi, kukua kwa uanzishwaji viwanda na mambo mengine mengi.

Kama wasemavyo wahenga, kidole kimoja hakivunji chawa, na kwa hiyo kama jitihada hizi zinazofanywa na BRELA hazitapokelewa na wananchi itakuwa ni sawa na kazi bure.

Watanzania wanapaswa kuchangamkia fursa zinazoambatana na urasimishaji wa biashara ikiwa ni pamoja na kupata haki za kipee za umiliki wa biashara.

Mfanyabiashara ana uwezo wa kuitangaza biashara yako katika soko la ushindani, kupata haki za kipee za kulinda ubunifu au uvumbuzi wako, kutambulika na Taasisi za kifedha mf. Benki wakati wa kufungua akaunti.

Kuongeza wigo wa kufanya biashara kubwa, biashara za kimataifa, kuongeza wigo wa kupata kazi na zabuni mbalimbali, kuaminika kwa wateja, pia kumewezesha mbunifu wa Alama kutambulisha na kutangaza bidhaa au huduma sokoni, kuwawezesha watumiaji wa bidhaa kuitambua na kuichagua kwa kuangalia Alama na mamboa megine megni.

Mtanzania, tembelea sasa www.brela. go.tz ukiwa na namba ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA), namba ya simu iliyo hai na anuani ya barua pepe iliyo hai ili kuweza kufungua akaunti yako na kupata huduma za BRELA na kama ukipata changamoto wasiliana na kituo cha huduma kwa Wateja kupitia

Na: Nehemia Mihayo

# Zifahamu faida 10 za kusajili Jina la Biashara




*Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni(BRELA), Bw. Godfrey Nyaisa (kulia) akimkabidhi cheti cha usajili wa Jina la Biashara. Bw. Brighton Rugora (kushoto), baada ya kukamilisha taratibu za usajili.*

Vitu vyote vikubwa ambavyo tunavishuhudia sasa, havikuanza kwa ukubwa huo -- vilianza katika hatua ya chini na vikaendelezwa mpaka kufikia hapo vilipo.

Ni bahati mbaya kwamba Waafrika wengi hatuna desturi ya kuanzisha vitu ambavyo vinaweza kuishi maisha marefu hata baada ya mwanzilishi kufariki. Hata hivyo hii inaweza kuwa ni kutokana na sababu nyingi

Inaendela uk 22

ikiwemo uelewa mdogo kuhusu masuala ya Biashara. Katika kuchambua hilo watu wengi hawafahamu faida zinazoambatana na usajili wa jina la biashara. Makala hii imeainisha faida 10 ambazo mfanyabiashara anafaidika nazo anapokuwa amesajili Jina la biashara yake.

## KUIPA BIASHARA UPEKEE

Kusajili Jina la Biashara kunaifanya biashara husika kuwa na upekee. Hii ni kwa sababu jina la biashara lililosajiliwa haliwezi kutumika kusajili biashara nyingine. Hii itawafanya wateja kuitambua kwa urahisi biashara yako, na hivyo kuongeza idadi ya wateja.

## HUSAIDIA KUITANGAZA BIASHARA

Kuitangaza biashara ambayo ina jina ni rahisi kuliko kutangaza biashara ambayo haina jina. Hii ni kwa sababu katika eneo moja wafanyabiashara zaidi ya watano wanaweza kuwa wanafanya biashara ya aina moja. Katika mazingira kama haya kitu pekee kinaweza kitofautisha biashara yako na biashara nyingine ni Jina la Biashara. Utofauti huu utasaidia pale unafanya matangazo na kuwaelekeza wateja katika eneo ambalo biashara yako wasipotee na kwenda katika biashara ya mtu mwingine.

## KUPATA MKOPO WA BIASHARA

Usajili wa Jina la Biashara unaipa uhai wa kisheria biashara yako, na kwa maana hiyo taasisi za fedha zinajenga uaminifu na uwepo wa biashara husika na hivyo kuweza kutoa mkopo kwa ajili ya uendelezaji wa biashara.

## UKUAJI WA BIASHARA

Mfanyabiashara au mjasiriamali anapokuwa amesajili jina lake la biashara baada ya hatua za ukuaji na ongezeko la mtaji anaweza kulitumia jina hilo hilo kusajili kampuni; hivyo kuwa amepiga hatua kubwa zaidi katika ukuaji wa biashara yake.

## KUIPATIA UTU WA KISHERIA BIASHARA

Kusajili Jina la Biashara kunaifanya biashara husika kuwa na utu wa kisheria, mathalani kufungua akaunti katika taasisi za fedha au kumshitaki au kushitakiwa na mtu au taasis baada ya kurasimisha. Katika mazingira haya ipo tofauti kati ya mmiliki wa biashara na biashara husika. Mfano, biashara ikishitakiwa na kutakiwa kulipa fidia, hiyo haitamhusu mwenye biashara bali biashara husika.

## NAMNA YA KUSAJILI JINA LA BIASHARA

Kwa Tanzania, Jina la Biashara husajiliwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), ambapo mwombaji atatakiwa kuwa na namba ya kitambulisho cha taifa. Mwombaji atatembelea www.brela.go.tz kufungua akaunti katika mfumo wa usajili kwa njia ya mtandao, kisha atatuma maombi yake BRELA na endapo amejaza taarifa zake kwa ufasaha katika siku moja pekee mwombaji anakuwa amepata cheti chake cha Usajili wa Jina la Biashara.

Na: Nehemia Mihayo

BRELA
WAKALA YA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI

BRELA
BUSINESS REGISTRATIONS AND LICENSING AGENCY



BRELA HOUSE Plot no. 23, Block no. 20,
Shaaban Rober Street Sokoine Drive, P.o Box 9393 Ilala, Dar es Salaam

BRELA tanzania    brela_tanzania    brela_tanzania

“Tunaipa utu wa kisheria biashara yako”